# TARGETER WINGS DARASA LA SITA -MWAKA 2021

# MTIHANI WA MJARABU

Wings 009

# KISWAHILI SEHEMU YA KWANZA

*MUDA: Saa1 dakika 40*

***Soma kifungu kifuatacho. Kina nafasi 1 mpaka 15. Kwa kila nafasi umepewa majibu manne. Chagua jibu lililo sahihi.***

Kusoma ni___1___ya stadi nne muhimu. Stadi hizo___2___ni kusikiliza, kuzungumza na kuandika. Kusoma si ___3___mdomo tu na kutoa sauti, eti bora usikike. La!___4___. Kusoma ni zaidi ya hiyo.

Msomaji___5___ni yule ambaye anahakikisha kuwa sauti___6___ inasikika vyema. Sauti___7___ yafaa itoke kwa ulaini fulani; yaani___8___kuparuza. Sauti inayoparuza haiwavutii wasikilizaji.___9___na sauti kusikika, matamshi bora ni muhimu. Msomaji___10___ anatakikana azingatie alama za uakifishaji. Hii ___11___ wasikilizaji___12___ujumbe bila matatizo___13___. Ifahamike kuwa___14___ ni namna ya sanaa, na sanaa ni urembo; naye ni nani asiyependa___15___.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 1. | A. moja ya | B. mojayapo | C. mojawapo | D. mojalapo |
| 2. | A. mingine | B. nyingine | C. vingine | D. wengine |
| 3. | A. kuziba | B. kugunga | C. kuzibua | D. kufungua |
| 4. | A. Hakuna | B. Hasha | C. Kamwe | D. Kabisa |
| 5. | A. mazuri | B. muzuri | C. mzuri | D. nzuri |
| 6. | A. yake | B. chake | C. zake | D. lake |
| 7. | A. zenyewe | B. mwenyewe | C. lenyewe | D. yenyewe |
| 8. | A. na | B. bila | C. kwa | D. pasipo |
| 9. | A. Juu | B. Karibu | C. Mbali | D. Pasi |
| 10. | A. lakini | B. kamwe | C. bali | D. pia |
| 11. | A. husaidia | B. imesaidia | C. ilisaidia | D. haisaidii |
| 12. | A. kusahau | B. kuelewa | C. kukumbuka | D. kuandika |
| 13. | A. lolote | B. yoyote | C. zozote | D. yeyote |
| 14. | A. uandishi | B. uchoraji | C. usomaji | D. uimbaji |
| 15. | A. ! | B. , | C. . | D. ? |

***Kutoka swali la 16 mpaka 30, jibu kulingana na maagizo.***

16. Ni sentensi gani iliyoakifishwa vizuri?
    A. Asante, umenisaidia sana.
    B. Asante, umenisaidia sana!
    C. Asante umenisaidia sana.
    D. Asante, umenisaidia sana?

17. Andika sentensi ifuatayo katika usemi halisi
    *Mwalimu aliwaambia wanafunzi kuwa wangechelewa wangeadhibiwa.*
    A. Ukichelewa utaadhibiwa,"mwalimu aliwaambia wanafunzi.
    B. "Wakichelewa wataadhibiwa," mwalimu aliwaambia wanafunzi.
    C. "Mkichelewa mtaadhibiwa," mwalimu aliwaambia wanafunzi.
    D. "Nikichelewa mtaadhibiwa," mwalimu aliwaambia wanafunzi.

18. Kanusha sentensi ifuatayo:
    *Miti yote imekatwa*
    A. Miti yote hijakatwa.
    B. Miti yote haijakatwa.
    C. Miti zote hazijakatwa.
    D. Miti yote hazijakatwa.

19. Watoto <u>wote</u> wamepita mtihani
    *Neno lililopigwa mstari ni* ______
    A. kivumishi kionyeshi.
    B. Kivumishi kimilikishi.
    C. Kivumishi cha idadi.
    D. Kivumishi cha pekee.

20. Amani anawapenda wana wake.
*Ufupisho wa maneno yaliyopigwa mstari ni* ___________
A. wanawe B. wanawake
C. wanaake D. wanao

21. Kutokana na kivumishi -zuri tunapata nomino
A. vizuri B. uzuri
C. mzuri D. nzuri

22. Katika mmea fulani binadamu hula ndizi naye ng'ombe hula ___________
A. maua. B. mdizi.
C. mizizi. D. mgomba.

23. Ni sentensi gani iliyotumia 'bora' kumaanisha afadhali
A. Mwanafunzi bora ametuzwa.
B. Kampuni hiyo inatengeneza bidhaa bora.
C. Shule ile inatoa elimu bora
D. Ni bora kunywa uji kuliko kulala njaa.

24. Ni sentensi gani imetumia kitenzi katika hali ya kutenda
A. Mwanafunzi amechelewa.
B. Mwizi anafukuzwa.
C. Mtoto mtundu amekemewa.
D. Maji yanachemshwa.

25. Ni neno gani halipatikani katika ngeli ya I-ZI
A. Shule. B. Sanduku.
C. Sahani. D. Nyumba.

26. Kucheza kwake kunafurahisha.
*Neno kucheza limepigwa mstari. Neno hilo ni*
A. kivumishi. B. kielezi.
C. kitenzi. D. nomino.

27. Kamilisha sentensi kwa tanakali za sauti sahihi
*Alijifunika kwa blanketi* ___________
A. gubigubi B. ndi
C. bingiribingiri D. pu

28. Mdudu ambaye hupendelea kujificha kwenye vitanda na viti na kuishi kwa kufyonza damu ya binadamu ni
A. kiroboto B. chawa
C. kunguni D. kupe

29. Kamilisha methali ifuatayo:
Asiyekujua ___________.
A. hakujali. B. hakudhamini.
C. hakuthamini. D. hakujui.

30. Chombo cha kivita kinachoweza kwenda chini kwa chini majini ni _______
A. nyambizi. B. manowari.
C. kifaru. D. jahazi.

***Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 31 mpaka 40.***

Mwalimu anapokuja darasani na kuwataka wanafunzi waandike insha, wanafunzi wengi hukasirika. Huona kuwa mwalimu anawasumbua. Wengi huona kuwa kuandika insha ni kupoteza wakati. Huwa hawaoni umuhimu wa insha.

Uandishi wa insha ni muhimu sana katika maisha ya sasa darasani, na hata baadaye nje ya darasa.

Darasani mwalimu huwa ana sababu mbalimbali zinazomfanya awatake wanafunzi kuandika insha. Sababu ya kwanza ni kuwa mwalimu hutaka kupima ufahamu ama ujuzi wa mwanafunzi katika lugha ya Kiswahili. Mwalimu hutaka kujua iwapo mwanafunzi anajua msamiati aina mbalimbali; maana na matumizi ya msamiati huo. Vilevile mwalimu hutaka kujua iwapo mwanafunzi anaweza kujieleza kwa kiswahili sanifu. Ujuzi wa mwanafunzi na lugha hudhihirika wakati mwanafunzi anatunga sentensi. Sentensi hizi huunda aya; Nazo aya huunda mtungo mzima, yaani insha. Sentensi sahihi lazima zizingatie sarufi na hasa ngeli.

Umuhimu wa insha nje ya darasa huonekana wakati mwanafunzi amemaliza shule. Baada ya kumaliza shule mwanafunzi huenda akasomea taaluma ya uanahabari. Hii ni taaluma inayohusiana na uandishi. Mwanahabari ni mtu anayeandika habari za magazeti. Yeye huishi kwa kuandika.

Wanahabari ni watu wenye ujuzi wa lugha. Ili kazi zao ziweze kupendwa na kusomwa ni lazima ziandikwe kwa kiswahili sanifu. Vilevile ni lazima ziwe zenye ubunifu wa hali ya juu, ili ziweze kuvutia wasomaji. Kufaulu kwa mwanahabari kunategemea misingi ya lugha iliyowekwa na mwalimu darasani. Aidha kunategemea mkazo aliouweka mwalimu juu ya uandishi wa insha bora.

Mbali na uadishi wa habari mwanafunzi huenda akaibuka kuwa mwandishi wa vitabu. Hebu fikiria kitabu cha hadithi kina kurasa ngapi? Bila shaka si ukurasa mmoja, kurasa mbili au tatu. Ni kurasa nyingi. Kumbuka kwamba mwandishi wa kitabu cha hadithi alianza na sentensi moja. Kisha sentensi zikaunde aya; nazo aya zikajaza kurasa kadhaa. Nazo kurasa zikaunda sura; nazo sura zikaungana na kuunda kitabu chenye kurasa mia

moja, mia mbili, mia tatu ama hata zaidi. Je, ingewezekanaje mwandishi kuandika kitabu chenye kurasa nyingi namna hiyo kama kwanza hangeanza insha? Safari ndefu huanza kwa hatua moja.

---

**31.** Mwalimu anapowataka wanafunzi waandike insha wengi wao

A. hufurahia. B. hucheka.
C. huchangamkia. D. hukasirika.

**32.** Kulingana na aya ya tatu mwalimu huwa ana sababu ngapi zonazomfanya watake wanafunzi waandike insha?

A. Sababu mbalimbali.
B. Sababu mbili.
C. Sababu tusizozijua.
D. Sababu zisizo na idadi.

**33.** Mwalimu anapowaambia wanafunzi waandike insha huwa anataka kupima mambo yafuatayo isipokuwa

A. ufahamu wa lugha.
B. ujuzi wa lugha.
C. kutofahamu lugha.
D. ujuzi wa msamiati.

**34.** Ujuzi wa mwanafunzi wa lugha hudhihirika wakati mwanafunzi __________

A. anapotunga sentensi.
B. anapoandika insha.
C. anapoandika aya.
D. anapoandika mtungo mzima.

**35.** Umuhimu wa insha nje ya darasa huonekana wakati mwanafunzi __________

A. ameanza shule.
B. ameanza kazi.
C. anaendelea na shule.
D. amemaliza shule.

**36.** Kulingana na aya ya nne mwanahabari huishi kwa __________

A. kusoma. B. kuandika.
C. kuchora. D. kuzungumza.

**37.** Ili kazi za wanahabari ziweze kupendwa na kusomwa ni lazima ziweze kuandikwa kwa kiswahili

A. kipya. B. cha kisasa.
C. sanifu. D. cha kale.

**38.** Mbali na uandishi wa habari mwanafunzi anaweza akaibuka kuwa

A. mwandishi wa vitabu.
B. msanii.
C. mpigaji picha.
D. mchoraji picha.

**39.** Mwandishi wa kitabu cha hadithi alianza na

A. hadithi moja.
B. aya moja.
C. ukurasa mmoja.
D. sentensi moja.

**40.** Kichwa kinachofaa hadithi hii ni

A. Umuhimu wa habari.
B. Umuhimu wa insha.
C. Umuhimu wa hadithi.
D. Umuhimu wa uandishi.

---

***Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 41 mpaka 50.***

Katika kijiji cha Mukuru Kayaba, kuliishi kijana mmoja kwa jina Vincent Ateya. Alisomea katika shule ya Msingi ya Mukuru. Shule hii ilianzishwa na mwanamke mzungu mtawa kwa jina Mary Kileen. Lengo la kuanzisha shule hii lilikuwa ni kuwasaidia watoto wa kijijini kupata elimu; elimu ambayo iliwakwepa kwa sababu ya wazazi wao kutokuwa na uwezo wa kuwalipia karo katika shule 'bora'.

Shule hii ilipoanzishwa haikuwa vile ilivyo sasa. Ilikuwa imejengwa kwa mbao na mabati na kuzingirwa kwa ua la miti na waya. Mazingira yake hayakuwa ya kuvutia na mwalimu yeyote hangetamani kufundisha huko, isipokuwa yule ambaye alitambua kuwa walimu ni wito; na amtumikiaye mtoto humtumikia Mungu.

Sasa hivi ukienda shule hiyo huwezi kuamini macho yako ukilinganisha na ile ya zamani. Ni mojawapo ya shule zenye majengo bora mashariki mwa jiji la Nairobi. Majengo ya madarasa ni ya mawe na sakafu zake ni za kupendeza. Aidha imezungukwa kwa ua imara wa mawe.

Siku moja nikiwa mwalimu wa Kiswahili wa darasa la saba, niliwapatia wanafunzi wangu insha; Vincet akiwa mmoja wao. Hivi ndivyo Vincent Ateya alivyosema katika insha hiyo kuhusu mwalimu wake wa Kiswahili: "Mwalimu Alwenya ni mtulivu na hana machachari mengi. Unaweza kudhani kuwa hana lolote analolifahamu; kumbe anakifahamu Kiswahili kwelikweli."

Baada ya kuisoma insha ya mwanafunzi huyo niliyatafakari maneno hayo. Niliona tu kuwa alinivika kilemba cha ukoka yaani alinipa sifa nisizostahili. Sikumwuliza jambo lolote. Mwaka uliofuata alifanya mtihani wa darasa la nane akafaulu vyema; somo lake bora lilikuwa Kiswahili. Alijiunga na shule ya upili na baada ya miaka minne akafuzu. Baada ya kukamilisha elimu yake ya sekondari alijiunga na chuo cha wanahabari ili kutimiza ndoto yake ya kuwa mtangazaji.

Katika safari yake ya elimu, Vincent hakumsahau mwalimu wake wa shule ya msingi ambaye ndiye aliyejenga msingi wake wa lugha ya Kiswahili. Mara kwa mara alimtafuta na kumwuliza mambo mbalimbali kuhusu lugha ya Kiswahili. Hata baada ya kufuzu na kuajiriwa kama mtangazaji aliendelea kudumisha uhusiano huo.

Vincent alianza kazi yake ya utangazaji katika shirika la utangazaji la KBC. Kisha baadaye akajiunga na shirika la redio Citizen. Alihamia katika shirika la redio la Milele, kwa muda mfupi kisha akarejea tena katika redio Citizen. Vincent amekuwa mtangazaji maarufu kwa sababu ya kipindi chake cha 'Jambo Kenya na Vincent Ateya'. Mara kwa mara amesikika akimtaja mwalimu wa Kiswahili. Manase Alwenya kama mwalimu aliyempa motisha wa kujifunza lugha. Sifa si kujisifu, sifa ni kusifiwa. Jambo hilo limenifanya kuwa mnyenyekevu kwani limelifanya jina langu kuwa kubwa kuliko nafsi yangu.

Vincent Ateya ni mmojawapo wa wanafunzi wachache ambao huwakumbuka walimu wao, ndio maana nimeonelea niandike wasifu huu kumhusu; kwani kwendako mema hurudi mema.

**41.** Lengo la kuanzisha shule ya Mukuru lilikuwa ni
A. kuwasaidia watoto wa mjini.
B. kuwasaidia watoto wa shule bora.
C. kuwasaidia watoto wanaoweza kulipa karo.
D. Kuwasaidia watoto wa kijijini.

**42.** Shule ilipoanzishwa ilikuwa imejengwa kwa
A. mbao na misumari.
B. mbao na mabati.
C. miti na udongo.
D. mawe na simiti.

**43.** Walimu hawakutamani kwenda kufundisha katika shule ya Mukuru kwa sababu
A. hawakuwa na mwito.
B. ya uhalifu uliokithiri.
C. ya mazingira yasiyovutia.
D. majengo duni.

**44.** Shule ya sasa ya Mukuru ina tofauti na ila ya zamani kwa yote yafuatayo isipokuwa
A. majeno ya mawe.
B. watoto tofauti.
C. sakafu za kupendeza.
D. ua wa mawe.

**45.** Mwalimu Alwenya alimfunza Ateya katika darasa la ngapi?
A. La nane.
B. La nne
C. La sita.
D. La saba

**46.** Kumvika mtu kilemba cha ukoka ni
A. kumvika aina ya kitambaa.
B. kumsenngenya akisikia.
C. kumtendea maovu.
D. kumpa sifa asizostahili.

**47.** Baada ya kukamilisha elimu ya sekondari Vincent alijiunga na
A. chuo cha ufundi.
B. shirika la utangazaji.
C. chuo cha uanahabari.
D. chuo cha walimu.

**48.** Vincent alianza kazi yake ya utangazaji katika shirika la habari la
A. NTV
B. KBC
C. Redio Citizen
D. Milele Fm

**49.** Vincent ni maarufu kwa sababu ya kipindi chake cha
A. Jambo Kenya.
B. Habari Kenya.
C. Mambo Kenya.
D. Amka Kenya.

**50.** Mwalimu Alwenya ameamua kuandika wasifu kumhusu Vincent Ateya kwa sababu sifuatazo isipokuwa
A. alikuwa mwanafunzi wake bora.
B. huwakumbuka walimu wake.
C. kwendako mema hurudi mema.
D. anapenda kusifiwa.